**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA**

**MSAJILI WA HAZINA**

**HOTUBA YA MHESHIMIWA PROFESA KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB) WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MIPANGO NA UWEKEZAJI KATIKA HALFA YA SIKU YA GAWIO 2026 TAREHE 30 JUNI 2026, IKULU- DAR ES SALAM**

***Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mgeni Rasmi;***

***Mheshimiwa Balozi Khamis Mussa Omar, Waziri wa Fedha;***

***Waheshimiwa Mawaziri mliopo;***

***Mheshimiwa Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi;***

***Mheshimiwa Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;***

***Mheshimiwa Masanja Kadogosa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma;***

***Makatibu Wakuu na Manaibu Katibu Wakuu;***

***Dkt. Fred Msemwa, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji (Uwekezaji);***

***Bwana Waheed Mohammad Ibrahim Sanya, Msajili wa Hazina, Zanzibar;***

***Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama;***

***Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi wa Taasisi za Umma;***

***Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma;***

***Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Kampuni ambazo Serikali ina umiliki wa hisa chache;***

***Ndugu Wanahabari;***

***Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana.***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

**Kazi na Utu. TUNASONGA MBELE!**

***Mheshimiwa Rais,***

Kwa heshima kubwa na mimi naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na kutuwezesha kushiriki katika hafla hii muhimu ya Siku ya Gawio 2026. Aidha, napenda kuipongeza Ofisi ya Msajili wa Hazina, Bodi za Wakurugenzi, Menejimenti na watumishi wa Taasisi za Umma pamoja na kampuni ambazo Serikali ina hisa kwa mafanikio makubwa yaliyowezesha kuongezeka kwa gawio na michango mingine kwa Serikali mwaka huu.

***Mheshimiwa Rais,***

Kaulimbiu ya mwaka huu isemayo **"Uwekezaji wa Umma wenye Matokeo: Nguzo ya Uchumi Shindani na Maendeleo Endelevu kuelekea Dira 2050"** inatukumbusha kuwa mafanikio ya uwekezaji wa Serikali hayapimwi kwa ukubwa wa mtaji uliowekezwa pekee, bali kwa matokeo yake katika maisha ya wananchi, ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa. Matokeo tunayoshuhudia leo yanaonesha kuwa uwekezaji wa umma ukiendeshwa kwa misingi ya uwajibikaji, ufanisi na utawala bora unaweza kuwa chanzo kikubwa cha mapato ya ndani na kichocheo muhimu cha maendeleo ya Taifa.

Mh Rais

Gawio tulilolikabidhi leo ni Shilingi Trilioni 1.32/= ikiwa ni ongezeko la asilimia 30% ukilinganisha na gawio lililokabidhiwa kwako mwaka uliopita wa 2025. Hata hivyo, ili kuendana na malengo ya Dira, mchango wa mashirika ya umma katika ***pato ghafi*** la Taifa unatakiwa ufikie **Shilingi Trilioni 200 na gawio kwa serikali lifike shilingi Trilioni 32** kwa mwaka ifikapo mwaka 2050. Hivyo bado tuna kazi kubwa mbele yetu katika kuongeza ubunifu na ushindani ili kufikia malengo ya Dira 2050.

***Mheshimiwa Rais,***

Tunapoelekea katika utekelezaji wa Dira 2050, matarajio yetu kwa Taasisi za Umma yanapaswa kuwa makubwa zaidi na kujikita katika mambo matatu:-

~~1.~~ Taasisi za umma zilizoanzishwa kwa lengo la kufanya biashara zinatakiwa kufuata misingi ya kibiashara katika kujiendesha na kuendelea kutengeneza faida.

~~2.~~ Taasisi za umma zilizoanzishwa kwa malengo ya kufanya biashara lakini zinaendeshwa kwa ruzuku ya serikali zizingatie kuwa ukomo wa Ruzuku ni June 2029. Taasisi hizo ziandae Mpango (Roadmap) ya kujiondoa katika ruzuku ya serikali.

~~3.~~ Kwa kutafsiri malengo ya Dira 2050, ifikapo mwaka 2050, taasisi zote za umma zinatarajiwa kuwa zimeongeza uzalishaji mara kumi (10) zaidi ukilinganisha na viwango vya sasa ili kuendana na malengo tuliyojiwekea katika Dira yetu mpya.

~~4.~~

***Mheshimiwa Rais,***

Matokeo tunayoshuhudia leo yanatupa matumaini makubwa kuwa Tanzania ina uwezo wa kujenga taasisi imara, zinazojitegemea, zinazoshindana na zinazozalisha thamani kwa wananchi. Hata hivyo, mafanikio haya yanapaswa kuwa mwanzo wa hatua mpya ya mageuzi na si mwisho wa safari.

Kwa upande wa Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji, tunaahidi kuendelea kushirikiana kwa karibu na Ofisi ya Msajili wa Hazina kuhakikisha kuwa uwekezaji wa umma unakuwa kichocheo kikuu cha ukuaji wa uchumi, ongezeko la mapato ya ndani, ushindani wa Taifa na utekelezaji wa Dira 2050.

Nakushukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wako wenye maono na msisitizo wako wa kuhakikisha kuwa uwekezaji wa umma unatoa matokeo yanayoonekana na yanayopimika kwa wananchi.

Baada ya maelezo haya, napenda kuchukua fursa hii kukukaribisha Mhe. Rais ili uongee na hadhira pamoja na wananchi katika siku hii muhimu ya Gawio 2026.

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

**Kazi na Utu.**